TANGAZO LA SERIKALI Na. 1006 la tarehe 6/12/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA MIJI),
(SURA YA 288)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 89(1))*

## SHERIA NDOGO YA VIBALI VYA SHUGHULI ZA KIUTAMADUNI YA HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM YA MWAKA 2024

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Vibali vya Shughuli za Kiutamaduni ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 2024.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha unahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya kibali;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"shughuli za kiutamaduni" maana yake ni shughuli yoyote halali yenye lengo la kuleta furaha ikijumuisha sherehe, michezo na muziki isipokuwa kusanyiko la misiba.

Wajibu wa kuwa na kibali

4. Mtu yeyote anayefanya shughuli ya kiutamaduni katika eneo la Halmashauri atapaswa kuwa na kibali cha maandishi kutoka kwa Halmashauri.

Utaratibu wa kuomba kibali

5.-(1) Mtu yeyote anayekusudia kufanya shughuli ya kiutamaduni katika eneo la Halmashauri anapaswa kutuma maombi ya kibali kwa Mkurugenzi kupitia kwa Afisa Mtendaji wa Mtaa husika kwa kujaza fomu maalum kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza.

(2) Maombi ya kibali yatalipiwa ada kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Pili.

(3) Endapo maombi ya kibali yatakataliwa, Halmashauri itamuarifu mwombaji kwa maandishi na kutoa sababu za kukataa kutoa kibali hicho.

(4) Endapo kibali kimetolewa na Halmashauri ikabaini kuwa kuna sababu za msingi za kuzuiliwa kwa shughuli ya kiutamaduni kabla au baada ya kuanza kwa shughuli hiyo, Halmashauri itamuarifu mwombaji kwa maandishi na kutoa sababu za kuzuiliwa kwa kibali kilichotolewa.

(5) Nakala ya kibali cha kufanya shughuli za kiutamaduni itawasilishwa kwa Mkuu wa Polisi wa Wilaya ikiwa imeambatishwa na stakabadhi ya malipo ya ada.

Wajibu wa mmiliki wa ukumbi

6.-(1) Kila mmiliki wa ukumbi wa muziki, burudani au baa atakuwa na wajibu ufuatao:

Sura ya 191

(a) kupiga muziki kwa kiwango cha sauti kilichoruhusiwa na kanuni za udhibiti wa kelele na mitetemo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira.;
(b) kuhakikisha kuwa mwanafunzi au mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane haingii katika ukumbi;
(c) kuonesha picha mjongeo au sinema kwa kiwango cha sauti kilichoruhusiwa na kanuni za udhibiti wa kelele na mitetemo katika Sheria ya Mazingira.

Vigezo vya utoaji kibali

7.-Halmashauri itatoa kibali iwapo itajiridhisha na mambo yafuatayo:

(a) shughuli ya kiutamaduni inayoombewa kibali haitasababisha uvunjifu wa amani;

(b) eneo litakalotumika kwa ajili ya shughuli ya kiutamaduni linaruhusiwa kwa shughuli inayoombewa kibali;

(c) kumbi za kiutamaduni zina usalama wa kutosha ikiwa ni pamoja na kuwepo kwa vifaa vya kuzimia moto, madirisha makubwa yanayoruhusu hewa kupita na milango inayofunguka kwa urahisi wakati wa dharura; na

(d) shughuli ya kiutamaduni haitakiuka maadili ya Mtanzania.

Marufuku

8.-(1) Itakuwa ni marufuku kwa-

Sura ya 13

(a) mmiliki wa ukumbi wa muziki, burudani au baa kumruhusu mtoto, mwanafunzi au mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane kuingia kwenye ukumbi wa muziki, burudani au baa kama ilivyozuiliwa katika Sheria ya Mtoto;

(b) mtu mwenye kibali kumruhusu mtoto, mwanafunzi au mtu yeyote aliye chini ya umri wa miaka kumi na nane kuingia au kuendelea kuwepo katika shughuli ya kiutamaduni baada ya muda ulioruhusiwa kuisha;

(c) mmiliki wa ukumbi wa burudani kuonesha picha mjongeo na sinema au kutumia sehemu yoyote kuonesha picha ambazo hazina maadili.

(2) Muda wa kuonesha picha mjongeo au sinema utaanza saa kumi kamili jioni hadi saa sita kamili usiku kwa siku za kazi, isipokuwa jumamosi, jumapili na siku za sikukuu itakuwa kuanza saa saba kamili mchana hadi saa sita kamili usiku.

Mamlaka ya kufanya ukaguzi

9.-(1) Afisa Mwidhiniwa atakuwa na mamlaka ya kuingia mahala panapofanyika shughuli ya kiutamaduni

au anapoamini kuna shughuli ya kiutamaduni inafanyika kwa lengo la kukagua iwapo shughuli hiyo ina kibali au inafanywa kwa kuzingatia masharti ya kibali kulingana na Sheria Ndogo hii.

(2) Katika kutekeleza mamlaka yake chini ya kanuni ndogo ya (1), Afisa Mwidhiniwa atakuwa na uwezo wa kutoa maelekezo yoyote ikiwa ni pamoja na kusitisha shughuli ya kiutamaduni kulingana na hali itakayobainika baada ya ukaguzi kufanyika.

Mkusanyiko wa watoto

10.-(1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kukusanya watoto kwa ajili ya shughuli yoyote ya kiutamaduni ndani ya Halmashauri bila kibali cha maandishi cha Halmashauri.

(2) Mkusanyiko wowote wa watoto uliopata kibali cha Halmashauri kwa mujibu wa kanuni ndogo ya (1) utafanyika siku za mapumziko kuanzia saa nne kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(3) Mtu yeyote aliyepata kibali cha mkusanyiko wa watoto atakuwa na wajibu wa kuhakikisha usalama wao kipindi chote cha mkusanyiko na kuhakikisha wanatawanyika kwa usalama kutoka katika eneo la mkusanyiko.

(4) Mzazi, mlezi au mtu yeyote mwenye mamlaka juu ya mtoto atakuwa ametenda kosa endapo atamruhusu mtoto kuhudhuria mkusanyiko usio na kibali cha Halmashauri.

Vibali visivyotozwa ada

11.-(1) Mikusanyiko ifuatayo itaombewa vibali bila kulipa ada-

(a) mikusanyiko ya kidini;
(b) misiba na mazishi;
(c) michezo ya watoto isiyotozwa; na
(d) mikusanyiko ya kisiasa.

Usafi wa mazingira

12.-(1) Mtu yeyote atakayeendesha shughuli za kiutamaduni ndani ya mamlaka ya Halmashauri atalazimika kufanya usafi ndani au nje ya eneo lililotumika katika shughuli ya kiutamaduni kwa kuondoa uchafu wote uliosababishwa na shughuli ya kiutamaduni.

(2) Mtu yeyote atakayeshindwa kutekeleza masharti ya kanuni ndogo ya (1) atalipa gharama ya uchafuzi wa mazingira kadri zitakavyokadiriwa na Halmashauri na gharama zingine ambazo Halmashauri itatumia katika kuondoa uchafu huo.

Muziki unaoleta kero

13. Mtu yeyote mwenye leseni ya biashara au aliyepata kibali cha shughuli za kiutamaduni atatakiwa kupiga muziki kwa kiwango cha sauti kilichoruhusiwa na kanuni za udhibiti wa kelele na mitetemo katika Sheria ya Usimamizi wa Mazingira kwenye eneo lake la biashara au aliloombea kibali.

Ukamataji wa vifaa

14.-(1) Halmashauri inaweza kukamata vifaa vitakavyokutwa katika shughuli ya kiutamaduni ambayo haina kibali au inaendeshwa bila kuzingatia masharti ya kibali.

(2) Vifaa vitakavyokamatwa chini ya kanuni ndogo ya (1) vitachukuliwa na kuhifadhiwa katika ofisi za Halmashauri au eneo lolote litakaloamuliwa na Halmashauri.

(3) Vifaa vilivyokamatwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii vitatakiwa kukombolewa ndani ya siku saba kuanzia tarehe ya kukamatwa baada ya hapo, Halmashauri inaweza kuuza vifaa hivyo kwa mnada baada ya kuomba na kupata idhini ya Mahakama.

(4) Mtu yeyote anayetaka kurejeshewa vifaa vilivyokamatwa chini ya Sheria Ndogo hii atawajibika kulipa gharama za ukamataji, usafirishaji na utunzaji wa vifa hivyo.

Makosa na adhabu

15. Mtu yeyote atakayekiuka masharti ya Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atawajibika kulipa faini isiyopungua shilingi laki mbili na isiyozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au vyote kwa pamoja.

Kufifilisha kosa

16. Mkurugenzi anaweza kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria

Ndogo hii kiasi kisichozidi shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa kwa hiari na kujaza fomu maalumu kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Tatu la Sheria Ndogo hii.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo TS Na. 532 la 2019

17. Sheria Ndogo ya Ada na Vibali vya Shughuli za Kiutamaduni ya Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ya Mwaka 2019 inafutwa.

*Tangazo la Serikali Na.1006 (Linaendelea.)*

JEDWALI LA KWANZA

(*Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(1)*)

MAOMBI YA KIBALI CHA SHUGHULI YA KIUTAMADUNI

1. Jina kamili la mwombaji ……………………………………………….

2. Anwani/ Namba ya simu ya mwombaji ……………………………..

3. Eneo ambalo tukio litafanyika : Mtaa…………………… Kata………….

4. Taja mahali ambapo shughuli itafanyika (Ukumbini au Nyumbani au Eneo la wazi): ………………………………………………………………………….

5. Aina ya Shughuli ya Kiutamaduni (Mfano: Harusi, ngoma, Tamasha au Matangazo au Promosheni au kupiga picha, Maulidi)

6. Saini ya Mwombaji ……………………………………..………………

7. Tarehe ya tukio/shughuli…………………………..……………………

*KWA MATUMIZI YA OFISI TU*

MAONI YA MTENDAJI WA MTAA ATAKAPOFANYIA SHUGHULI YA KIUTAMADUNI
………………………………………………………………………
..........................................................................................................................
Tarehe ………………………………..Muhuri……………….…………………

Jina la Mtendaji wa Mtaa ……………………… Saini…………………….….

MAONI YA AFISA MTENDAJI WA KATA ATAKAPOFANYIA SHUGHULI YA KIUTAMADUNI
…………………………………………………………………………
.............................................................................................................................
Tarehe ………………………………Muhuri……………….………………

Jina la Afisa Mtendaji wa Kata ……………………… Saini…………………….…

MAAMUZI YA AFISA MWIDHINIWA

Maombi ya Kibali yamekubaliwa au yamekataliwa kwa sababu
...........................................................................................................................
…………………………………………………………………………
Unaruhusiwa kufanya shughuli ya kiutamaduni kuanzia saa …………. hadi saa ………..
Tarehe …………………………….. Muhuri …………….……………

Jina la Afisa Mwidhiniwa ……………………Saini…………………….….

MHASIBU
Kiasi: …………………………………. Risiti Na: ………………
Tarehe:…………………….. Sahihi:………………..…..
Muhuri

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 5(2))*

ADA YA KIBALI CHA SHUGHULI YA KIUTAMADUNI

| Namba | Aina ya Shughuli ya Kiutamaduni | Ada kwa kila Onesho au Tukio (shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Tamasha la muziki | 100,000/= kwa siku |
| 2 | Onesho la michezo ya kuigiza | 30,000/=kwa siku |
| 3 | Muziki wa disko | 30,000/=kwa siku |
| 4 | Muziki wa taarabu | 30,000/=kwa siku |
| 5 | Sherehe za mashirika na taasisi mbalimbali | 50,000/=kwa siku |
| 6 | Onesho la sinema (Isipokuwa maonesho ya kidini) | 50,000/=kwa siku |
| 7 | Sherehe nyinginezo | 30,000/=kwa siku |
| 8 | Upigaji picha jongefu | 30,000/=kwa mkanda |
| 9 | Upigaji picha mnato | 20,000/=kwa siku |
| 10 | Tamasha la ngoma za asili | 20,000/=kwa siku |
| 11 | Maonesho ya Sanaa au vichekesho | |
| | (a) kwa wageni kutoka nje ya nchi | 100,000/= kwa siku |
| | (b) kwa Watanzania | 20,000/= kwa siku |
| 12 | Mchezo wa mezani (pool table) unaochezeshwa kibiashara | 50,000/= kwa mwaka |
| 13 | Bahati nasibu | 30,000/= kwa mwezi |
| 14 | Korokoro au tombola au fete | 30,000/= kwa mwezi |
| 15 | (i) Matumizi ya uwanja wa mpira kwa ajili ya mashindano | 50,000/= kwa tukio |
| | (ii) Matumizi ya uwanja wa mpira kwa ajili ya burudani au mazoezi ya taasisi, mashirika au kampuni | 50,000/= kwa tukio |
| 16 | Betting | 50,000/= kwa mwezi |
| 17 | Bahati nasibu ya sanduku | 100,000/= kwa mwezi |
| 18 | Studio ya kurekodi sanaa | 100,000/= kwa mwaka |
| 19 | Sanaa za ufundi | 20,000/= kwa mwezi |
| 20 | Mashindano ya urembo ndani ya wilaya (Isipokuwa kwa mashindano yanayolenga kuibua vipaji na siyo kuingiza kipato) | 50,000/= kwa tukio |
| 21 | Mashindano ya urembo kitaifa (isipokuwa kwa mashindano yanayolenga kuibua vipaji na siyo kuingiza kipato) | 100,000/= kwa tukio |
| 22 | Matangazo mitaani kwa kutumia spika | 50,000/= kwa siku |
| 23 | Majengo ya biashara yanayoonesha picha mjongeo au picha jongefu mitaani | 20,000/= kwa mwezi |
| 24 | (i) Huduma za kumbi za starehe au burudani au sherehe | |
| | (a) Mapambo | 30,000/= kwa tukio |
| | (b) Chakula | 30,000/= kwa tukio |
| | (c) Muziki | 30,000/= kwa tukio |
| | (d) Mshehereshaji | 30,000/= kwa tukio |

*Tangazo la Serikali Na.1006 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| | (ii) Huduma za Kumbi kwa shughuli nyinginezo | |
| | (a) Mapambo | 30,000/= kwa tukio |
| | (b) Chakula | 30,000/= kwa tukio |
| | (c) Muziki | 30,000/= kwa tukio |
| | (d) Mshehereshaji | 30,000/= kwa tukio |
| 25 | Ada ya usajili | |
| | (i) Ada ya Usajili wa Vilabu na vyama vya michezo | 20,000/= kwa mwaka |
| | (ii) Ada ya Usajili wa kampuni ya ukuzaji michezo na mawakala wa ukuzaji michezo (sports promotion) | 30,000/=kwa mwaka |

JEDWALI LA TATU

*(Limetengenezwa chini ya kanuni ya 16)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ........................................................................nakiri KWA HIARI YANGU MIMI MWENYEWE mbele ya........................................................... ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kwamba tarehe ..........ya mwezi .................. Mwaka................ nilitenda kosa kwa kukiuka masharti ya kanuni ya ……..ya Sheria Ndogo ya Vibali vya Shughuli za Kiutamaduni ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam ya Mwaka 2024.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam, NAKUBALI kulipa kiasi cha shilingi ..................... ya ada ninayodaiwa pamoja na faini ya kufifilisha kosa ya shilingi ........................

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo hii tarehe .......................ya Mwezi ................................Mwaka …......…
Jina: .....................................................  Saini: .................................................

MBELE YA MKURUGENZI:
Jina.……....................................................
Saini: .........................................................
Tarehe: ....................................................

Lakiri ya Jiji la Dar es Salaam imegongwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia Azimio lililopitishwa katika Mkutao wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam uliofanyika tarehe 6/3/2023 na kushuhudiwa Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya:-

JOMAARY MRISHO SATURA,
*Mkurugenzi wa Jiji,*
*Halmashauri ya jiji,*
*Dar es salaam*

MHE. OMARY KUMBILAMOTO,
*Msahiki meya,*
*Halmashauri ya jiji,*
*Dar es salaam*

L.S

**NAKUBALI**,

Dodoma,
29 Agosti, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi OR-Tamisemi*